BISMILLAHIR RAHMANIR RAHIM.

Al hamisi tarehe13/Muharram/1427 H =01/02/2007 AD,Pongwe-Tanga,Tanzania.makala namba 10.

HII NDIYO DAAWA YETU

JUU YA MANHAJI YA SALAF SWALIH.

# ITIKADI YA IBIN SINA (AVICENNA) KATIKA MIZANI YA AHLIS SUNNA.

Amesema Imamu ad Dhah'by;
Al Hussein bin Abdillahi Ibin Sina,Abu Ally ar Raisy;
Sijui kama amepokea kitu chochote katika elimu-za hadithi- na hata kama angepokea isingekuwa halali kupokea kutoka kwake,kwasababu yeye alikua ni mtu wa falsafa,na ni mpotevu,na ALLAH ASIWE RADHI NAYE!!!!
Lisanul mizani juz 1,uk291.

MUANDISHI;

ABUL FADHLI QASSIM MAFUTA QASSIM AL SALAFY.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote,
ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.
Ama baada ya utangulizi.

Katika misingi ya itikadi sahihi ya Ah'lis Sunna wal Jamaa,na Man'haji sahihi ya Salaf Swalih ni kupendana na kunusuriana kwasababu ya kushikamana na itikadi sahihi,na kutengana,na kuchukiana kwasababu ya kuihalifu itikadi hiyo sahihi,na msingi huu unajulikana kama msingi wa (AL WALAU WAL BARAU).

Na ni makosa makubwa kwa watu kupendana na kuchukiana kwasababu zisizokuwa za kidini.
Na kwa msingi huu wa Al walau wal barau kuna patikana ulazima wa kuwatambua watu walio kinyume na itikadi ya Ah'lis Sunna,na Man'haji ya Salaf Swalih iliwachukiwe kwa kadri ya Bid'a zao,wachilia mbali kutukuzwa na kuadhimishwa!

Vile vile kuna ulazima wa kuzibainisha itikadi,na fikra zao potofu na kuzirudi.
Bali na kuwarudi wote wenye kuwatetea,na kuwaadhimisha,au kuziadhimisha fikra zao,na vitabu vyao na kuwaenzi !
Bali na hata wale wenye kuchukia kutajwa vibaya vingunge hao wa Bid'a!!

Amesema Sheikhul Islamy Ibin Taymiyyah-Allah amrehemu-katika Maj'muu fatawa 2/132 ;

**ويجب عقوبة كل من انتسب اليهم أو ذب عنهم أو أثنى عليهم أوعظم كتبهم أو عرف بمساعدتهم ومعاونتهم أو كره الكلام فيهم أو أخذ يعتذر لهم..... بل تجب عقوبة كل من**

عرف حالهم ولم يعاون على القيام عليهم فإن القيام على هؤلاء من أعظم الواجبات ....

Ni wajibu kumuadhibu kila mwenye kujinasibisha na(watu wa bid'a) au kuwatetea au kuwasifia au kuviadhimisha vitabu vyao au aliye julikana kuwapa msaada

**Au akawa anachukia kusemwa (hao watu wa bid'a) na akawa anawapa nyudhuru……**

bali ni wajibu kumuadhibu kila mwenye kuijua hali yao (ya bid'a) kisha asisaidie kupambana nao,kwasababu kupambana nao ni katika wajibu ulio mkubwa….

## SABABU YA KUANDIKA MAKALA HII

Miongoni mwa watu wa Bid'a wanao adhimishwa,na kutukuzwana kuenziwa,tena hata na wale watu wanao jinasibisha na Sunna na kuitetea –hasa katika mambo ya furuu (matawi) - ni huyu Ibin Sina.

Ibnu Sina anaadhimishwa,na kuenziwa mpaka kufikia baadhi ya jumuia na taasisi za kidini tena zilizo kua katika mrengo wa Sunna – k.v.AMYC- wamefikia kuziita baadhi ya

Shule zao kwa jina lake ili kuhuisha utajo wake,na kuzienzi fikra zake!! na kujenga mapenzi juu yake hasa kwa watoto wanao walea katika shule hizo !!!

Na jambo hili ni kinyume na uislamu,kinyume na man'haji ya Ahli Sunna,na pia ni jambo la hatari kwa malezi ya watoto hao wanaosoma shule hizo na kwa kizazi kijacho ambacho kinatarajiwa kuinusuru Sunnah juu ya Man'haji sahihi ya Salaf Swalih.
Na hakuna kilicho nipelekea kuandika makala hii isipokuwa sababu hizi zifuatazo;

1)kuwatanabahisha waislamu juu ya hatari,na ubaya wa jambo hili, na kuulinda mustaqbali wa watoto wa kiislamu ambao ni watetezi wa dini hii,na Man'haji hii sahihi.

2)ukaidi wa wahusika baada ya kunasihiwa.

3)kuzibatilisha baadhi ya kauli -ambazo si rasmi- zinazo tolewa na wahusika kwamba eti Ibnu Sina ametubia,kwahiyo hakuna ubaya kuita shule kwa jina lake!

## Vipi tuamiliane na ahlul bid'a?

Kwa msimamo wa Ah'li Sunna wal Jamaa haifai kumtukuza mtu wa bid'a na kumuadhimisha,-hasa yule mwenye kujua,na akawa analingania katika bid'a- bali ni wajibu kumtaja vibaya,na kuwatahadharisha watu na ubaya wake,na vitabu vyake,na fikra zake Amesema Ibnu Taymiyyah;

ومثل أئمة البدع من أهل المقالات المخالفة للكتاب والسنة او العبادات المخالفة للكتاب والسنة فان بيان حالهم وتحذير الأمة منهم واجب باتفاق المسلمين

Na mfano wa wanawachuoni wa bid'a wenye maneno yenye kukhalifiana na kitabu,na Sunna,au ibada zenye kuhalifiana na kitabu na Sunna,kwahakika kubainisha hali zao,na kuutahadharisha umma na wao ni jambo la wajibu kwa mapatano ya waislamu wote. Majmuu fatawa juzuu 28/231-232.

قال شيخ الإسلام ابن تيمية:

**فلا بد من التحذير من تلك البدع وان اقتضى ذلك ذكرهم وتعيينهم**

**......**

**الفتاوى 233/28.**

Amesema tena;
Ni lazima kutahadhirisha bid'a zote,ijapo kuwa hilo litapelekea kuwataja majina (basi watajwe)....
Maj'muu fatawa 28/232.
Haifai kuwaadhimisha watu wa bid'a,amesema Imamu Fudhail bin Iyadh;

**(( من عظم صاحب بدعة فقد أعان على هدم الإسلام...))**

**شرح السنة للبربهاري ص 139.**

Mwenye kumuadhimisha mtu wa bid'a atakuwa amesaidia juu ya kuuvunja uislamu.
Shar'hu Sunna cha al Bar'bahary uk 139.
Na bila shaka Ibnu Sina ni mtu wa bud'a,na wala si mtu wa Sunna,na kuiita Shule kwa jina lake ni kumuadhimisha,na wala si kumdhalilisha.
Haifai kuwanyamazia watu wa bid'a,amesema Ibnu Taymiyyah;

وقال بعضهم لاحمد ابن حنبل انه يثقل على أن أقول فلان كذا وفلان كذا فقال:

(( اذا سكت أنت وسكت أنا فمتى يعرف الجاهل الصحيح من السقيم))

مجموع الفتاوى28/231–232.

Wamesema baadhi yao kumuuliza Imamu Ah'mad bin Hanbal;
Kwahakika inakuwa uzito kwangu kusema;fulani kadha,fulani kadha,akasema;

Ukinyamaza wewe,na nikinyamaza mimi ni lini atajua mtu mjinga,sahihi na mbovu.maj'muu fatawa 28/231-232.
Bali haifai hata kukaa na watu wa bid'a,amesema al Fudhail bin Iyadh;

لا تجلس مع صاحب بدعة فإني أخاف أن تنزل عليك اللعنة

Usikae na mtu wa bid'a,mimi naogopea isije kukushukia laana!

Mtu wa bid'a hana toba mbele ya Allah s.w.t.
amesema  Sufyan atThaury;

البدعة أحب إلى إبليس من المعصية،المعصية يتاب منها والبدعة لا يتاب منها.))

شرح أصول السنة للالكائي**1/149**.

((Bid'a inapendeza zaidi kwa Iblisi kuliko maasi,mwenye maasi hukubaliwa toba-akitubia-(lakini) mtu wa bid'a hakubaliwi toba yake-mpaka aache bid'a yake-))Sharhu usuli Sunna 1/149.

Ukimsengenya mtu wa bid'a kwasababu ya bid'a yake hupati dhambi,
amesema Imam Ah'mad;

وقال الإمام أحمد :((لا غيبة لأصحاب البدع)).طبقات الحنابلة**2/274**.

Hakuna –dhambi- kwa kuwasengenya watu wabid'a.
Twabaqatul Hanabila 2/274.

Bali ni wajibu kuwatenga,na kukaa nao mbali,amesema Ibnu Taymiyyah;

قال شيخ الإسلام:

فبهذا أو نحوه رأى المسلمون أن يهجروا من ظهرت عليه علامات الزيغ من المظهرين للبدع الداعين إليها والمظهرين للكبائر.
فأما من كان مستتراً بمعصيته أو مسرًا لبدعة غير مكفرة،فإن هذا لايُهجر ...)) الفتاوى 24/174–175.

Na kwasababu hii au mfano wake wameona waislamu kuwafanyia hajri –kuwahama-wale wenye kudhihiri juu yao alama za bid'a na upotofumiongoni mwa ,wale wenye kudhihirisha bid'a,wenye kulingania kwenye bid'a,na kudhihirisha madhambi makubwa. Ama mwenye kujificha kwa maasi au bid'a isiyo kufurisha,mtu huyu hato fanyiwa hajri(hato tengwa)…." majmuu fatawa 24/174-175

## NI IPI ITIKADI YA IBNU SINA?

Baada ya kuujua msimamo halisi wa Ahli Sunna,sasa hebu tuiangalie Itikadi ya Ibin Sina (Avicenna),je itikadi yake ni itikadi sahihi kwa misingi ya Ahli Sunna?

Jawabu lake ni la.bali itikadi yake ni potofu,na ni kinyume na itikadi ya

kiislamu,kiasi ambacho wamefikia wanawachuoni wakubwa waliokua katika zama zake na waliokuja baada yake kumkufurisha na kumtoa nje ya uislamu!!

Na hizi zifuatazo ni baadhi ya kauli za baadhi ya maulamaa wakubwa wa kiislamu katika zama zake na walio kuja baada yake;

1- Amesema Imamu ad Dhah'by;

الحسين بن عبد الله بن سيناء أبو علي الرئيس:
ما أعلمه روى شيئا من العلم ولو روى لما حلت الرواية عنه لأنه فلسفي النحلة ضال لا رضي الله عنه انتهى

Al Hussein bin Abdillahi Ibin Sina,Abu Ally ar Raisy;
Sijui kama amepokea kitu chochote katika elimu-za hadithi- na hata kama angepokea isingekuwa halali kupokea kutoka kwake,kwasababu yeye alikua ni mtu wa falsafa,na ni mpotevu,na ALLAH ASIWE RADHI NAYE!!

Lisanul mizani juz 1,uk291.

2-Na amesema al Hafidh Ibin Hajar;

فقطع علماء زمانه ومن بعدهم من الأئمة ممن يعتبر قولهم أصولا وفروعا بكفره ....

Wamepitisha hukumu wanawachuoni wa zama zake,na waliofuatia baada yao, miongoni mwa wanawachuoni wanaotegemewa kauli zao katika mambo ya misingi na matawi juu ya ukafiri wake!!!!
Tazama lisaanul mizani juz 1,uk293.

3-Na amesema al Imamu Ibin Kathir;

وقد أطلق الغزالي وغيره القول بتكفير بن سيناء
Na ametoa hukumu Imamu al Ghazaly na wengineo juu ya ukafiri wa Ibin Sina…!!!
Tazama al bidayatu wannihayat juz12,uk489.
Na amesema Imamu Ibnul Qayyim;
واتخذ للملاحدة مدارس ورام جعل إشارات إمام الملحدين ابن سينا مكان القرآن .....
وبالجملة فكان هذا الملحد هو وأتباعه من الملحدين الكافرين بالله وملائكته وكتبه ورسله واليوم الآخر...
Na akawajengea Mul'hidina madarsa,na akataka kuziweka ishara za imamu wa mul'hidina Ibin Sina mahali pa Qur'an…..kwa ujumla –ni kwamba –alikua Mul'hidi huyu na wafuasi wake ni katika Mul'hidina wenye

kumkufuru Mwenyezi Mungu,na Malaika wake,na Vitabu vyake,na Mitume yake,na Siku
ya mwisho….))
tazama Ighaathatul lah'fani juzuu ya 2,ukurasa 531-535.

Na amesema Sheikhul Islami Ibin Taymiyyah;
....وهذه طريقة الإيمان من بعض الوجوه وإن لم يكن مؤمناً الفارابى وابن سينا لكن ابن سينا

…..na hii ndiyo njia ya al Faraby,na Ibin Sina,lakini Ibin Sina yuko karibu zaidi katika imani kuliko baadhi ya njia,ijapokuwa si muislamu..!!!!!
Maj'muu fatawa 12/22.

Amesema tena Ibin Taymiyyah;
كان فقهاء بخارى يقولون فى ابن سينا كان كافرا ذكيا...40/9 مجموع الفتاوى.
Walikuwa wanawachuoni wa Bukhara wanasema kuhusu Ibin SINA kwamba;
alikuwa KAFIRI mwerevu!!
Maj'muu fatawa 9/40.

وكذلك ابن سينا وغيره يذكر من التنقص بالصحابة ما ورثه من أبيه وشيعته القرامطة"
....."
مجموع الفتاوى103/4

Vile vile Ibin Sina na na wengineo wanawataja Maswahaba kwa kuwatukana kwa yale aliyo yarithi kutoka kwa baba yake na wenzake katika Qaramita….
Maj'muu fatawa 4/103.

Huyo ndiye Ibnu Sina anaye enziwa na baadhi ya wanao jinasibisha na Sunna!!

## KWANINI IBNU SINA AMEKUFURISHWA?

Maulamaa wakubwa wa Ah'li Sunna na wengineo wamefikia kumtia ukafirini Ibnu Sinna,si kwa kumonea bali ni kwasababu ya itikadi zake potofu,amesema Imamu Ibnu Kathir;

قد حصر الغزالي كلامه في مقاصد الفلاسفة ثم رد عليه في تهافت الفلاسفة في عشرين مجلسا له كفره في ثلاث منها

– وهي قوله يقدم العالم

– وعدم المعاد الجثماني

– وان الله لا يعلم الجزئيات

–وبدعه في البواقي

Na al Ghazaly ameyadhibiti maneno yake katika (kitabu chake) Maqasidul falasifa,na kumrudi katika kitabu Tahafutil falasifa katika maj'lis ishirini,na kumkufurisha katika majlisi tatu,katika hizo ni;

-kauli yake kwamba ulimwengu ni wakale(na hauna mwanzo)

-kupinga kufufuliwa viwiliwili (siku ya Qiyama)!!

-na kwamba Allah s.w.t. hayajui mambo kwa juz'iyyaati (upambanuzi)!!

-na akamtia katika bid'a kwa mambo yaliyo bakia.

Tazama al bidayatu wannihayat juzuu ya 12/ukurasa 489.

Bila shaka mwenye kuitakidi kwamba ulimwengu hauna mwanzo, atakuwa amekufuru.
Sambamba na yule mwenye kuitakidi kwamba viwiliwili havito fufuliwa siku ya Qiyama,na yule anaye mnasibishia Allah s.w.t. ujinga !!

Pamoja na hayo yote Ibin Sina alikuwa ni katika Qaramita-na nikisema hivi wale waliokuwa na ufahamu juu ya mapote wanafahamu- na alikuwa akiwatukana maswahaba wa Mtume s.a.w.!

## Wasemvyo watetezi wa Ibin Sina

Pamoja na kauli zote hizo za maulamaa wa Ah'li Sunna kuhusu Ibin Sina bado kuna baadhi ya ndugu zetu katika uislamu wanajaribu kumtetea,bali kumuadhimisha,na kumuenzi !!! kwa hoja eti kuna baadhi ya wanawachuoni wamesema kwamba;kabla ya kufa kwake alioga,kisha akaswali,na kutubu kwa Allah !

Kauli hii wameitaja wanawachuoni kama k,v. ad Dhah'by,Ibin Hajar, na Ibin Kathir,lakini Ibin Kathir ameitilia shaka kauli hii juu ya usahihi wake,na akaitaja kwa tamko la kuidhoofisha kwa kusema;

ويقال إنه تاب عند الموت فالله أعلم

((Na inasemekana kua ametubia wakati wa kufa kwake Allah anajua zaidi..)).

Na bila shaka tamko hili kwa wale wenye ufahamu wa mambo ya elimu za mustalahul Hadithi wanafahanu linaleta maana gani?

Ama suala la kua eti alioga,akaswali,kisha akatubu kwa mola wake, au kua alitamka kalima ya Shahada kabla ya kufa, hilo hatuwezi kulipinga-pamoja na kua kuthibiti kwake kuna mashaka- lakini iko wapi misingi ya Ah'li Sunna kuhusiana na mtu aliye kufuru kwa jahari,na kuutetea ukafiri huo kwa juhudi zote katika maisha yake yote.
kisha atubie chini ya uvungu wa kitanda chake **bila ya kuyakana na kujitakasa na yote aliyokuwa akiyaitakidi?!**

Na kwasababu kufanya hivi ni kinyume na itikadi sahihi ya Ah'li Sunna,
Ndiyo maana maulamaa wakubwa wa Ah'li Sunna katika zama zake na waliokuja baada yake –k,v. Ibnu Taymiyyah,ad Dhah'by, Ibnul Qayyim, Ibinu Kathir na wengineo hawakuizingatia toba yake hiyo, mpaka kufikia Imamu ad Dhahby kusema;
Allah asiwe radhi naye…!!!
Na Ibnul Qayyim kumuita kuwa ni Imamu wa makafiri..!!!

Kwahiyo tunashangazwa na hawa ndugu zetu wanao jinasibisha na Sunna na kudai kuitetea vipi wanamuenzi mtu kama huyu,na wanapo kumbushwa wanakuwa wakali na wakawa wanatafuta kila njia za kumtetea,kwa madai eti alikua Daktari bingwa !! mpaka makafiri pia wanakiri hilo!

**Lakini hawaelezi,wala hawachunguzi ni ipi ilkua itikadi yake?**

Kwasababu itikadi kwao si muhimu,na hisia zao zimekufa katika kupenda mno secular mpaka wamepofuka macho hawaoni tena uzito wa tofauti za kiitikadi!!

Iko wapi Sunna?!
Iko wapi al walau wal barau?!

Mara Ibnu Batuta(Sufy,Qubuury khurafy)

Mara Ibnu Sina(Imamul mulhidin,Qur'mutwiyyun)

Wako wapi maulamaa wa Sunna?!(k,v.Ibnu Taymiyyah,Ibnul Qayyim,Ibnu Kathir,Albany,Ibnu Baaz,Ibnu Uthaymin n,k.)?!

Mnafikiri ninani atakaye waenzi maulamaa hawa-wa Sunna- kama siyo sisi tunaojinasibisha na Sunna?!

## Khatima

Mwisho tunatarjia kuwa wahusika hawatofanya ukaidi,na kuanza kumtetea mulhid huyu,bali watafuata misingi ya Ah'li Sunna katika kuamiliana na watu wa bid'a,hasa kama bid'a ya huyu Ibni Sina ambayo imemfikisha katika ukafiri-Allah atukinge na kufru baada ya uislamu-

Hizo kauli zinazo sema kwamba ametubia maulamaa wa kubwa k,v.Ibnul Qayyim,ad Dhah'by Ibnu Kathir n,k. wameziona lakini ima kwa **kutokusihi kwake,au kwa kutoyarudi,na kujitakasa na itikadi yake hawakuzizingatia kauli hizo.**

Maana katika misingi ya Ah'li Sunna toba ya aliyefanya madhambi jahara,na kuyatetea kwa kuandika vitabu ni kutubia jahara **na kuyakana aliyokuwa akiyaitakidi,kama alivyo fanya ar Razy,na al Ghazaly n.k.**

Ama kutubia chini ya uvungu wa kitanda huku fikra zako,na vitabu vyako vinawapotosha watu,kwa misingi sahihi ya Ahli Sunna bado tunalazimika kuamiliana naye kama mtu wa bid'a/kafiri.

Ushauri;
Baadhi ya ndugu zetu wamejaribu kutoa ushauri kwamba kwanini lisiongezwe neno (RI) kati ya SI – na NA,ikawa IBNU SIRINA,mwanwachuoni mkubwa katika Taabiina(walio wadiriki Maswahaba) fitna

ikaisha,badala ya kumng'ang'ania mtu ambaye kwa uchache ni mzushi ?!

## MAKALA; HII NDIYO DAAWA YETU !!

-Ni Makala zinazo walingania wislamu kurudi na kushikamana na kitabu cha Allah,na Sunna sahihi za Mtume s.a.w. juu ya ufahamu wa wema walio tangulia.

-Kuwalingania watu kuzibadilisha nafsi zao kwanza kimatendo,na kuzisafisha nyoyo zao,jamii zao  na ushirikina,bid'a,ufuska,na kuitanguliza dunia mbele kuliko mapenzi ya dini.

-Malezi bora juu ya misingi ya Tawheed,kufuata mafundisho ya Mtume s.a.w. kwa vitendo.

-Kuhuisha maadili mema ya kiislamu,na kuzipiga vita tamaduni,na maadili yote maovu.

-Kuwajenga watu juu ya misingi ya kielimu,badala ya kuwatia hamasa zisizo na msingi wowote na harakati hewa.
-Kuleta mshikamano wa kweli wa kiroho kwa kujifunga sote na mafundisho ya Qur'an,na Sunna juu ya ufahamu wa SALAF SWALIH.
-Kupiga vita mishikamano yote feki,mishikamano ya viwiliwili na hali nyoyo ziko tofauti,kama umoja wa mayahudi, "Utawadhani wako pamoja;kumbe nyoyo zao ni mbalimbali.Hayo ni kwasababu  wao ni watu wasio  na akili" Al hashr(59) aya ya 14.
-Kuwahimiza waislamu kushikamana na haki,na kuwa na subra juu ya yote yanayo wasibu,kwa kushikamana na hayo bila shaka faraja iko karibu.
Kuwahimiza watu kurudi kwa maulamaa walio katika haki,maulamaa wa ki Salaf katika zama hizi,pale inapo bidi kufanya hivyo,na kujiepusha na wababaishaji.

والله الموفق والهادي إلى سواء السبيل

وصلى الله وسلم وبارك على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين

والحمد لله أولاً وآخراً